

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA**

Telegrams "AFYA", DODOMA
Nambari ya simu: +255-026-
2323267/2351196
Nukushi Na: +255-22-213806



Mji wa Serikali - Mtumba,
Barabara ya Afya,
S. L. P 743,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

**UFAPANUZI KUHUSU HOJA ZILIZOTOLEWA KUHUSIANA NA
WAOMBAJI WA AJIRA WALIOITWA KAZINI.**

Dodoma, Juni 30, 2023.

Kufuatia hoja zilizoibuliwa na waombaji wa ajira kwenye tangazo la kuitwa kazini kwa wataalam 356 wa kada za afya lililotolewa **Juni 28, 2023**, Wizara ya Afya inapenda kutoa ufafanuzi wa masuala kadhaa yaliyowasilishwa na waombaji wa ajira.

Kupitia kibali cha ajira za Watumishi Kada za Afya kilichotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUU) chenye **Kumb. Na. FA.97/128/01"B"/72 cha Aprili 20, 2023**, na Kibali mbadala chenye **Kumb Na FA.97/128/01"B"/75 cha Mei 4, 2023** ilizitangaza nafasi hizo kwa ajili ya waombaji wenye sifa kutuma maombi yao.

Jumla ya maombi yaliyopokelewa kupitia mfumo wa ajira yalikuwa **16,423**, (Wanaume ni **9,354** na Wanawake **7,069**) kati yao waombaji **3,350** hawakujaza taarifa zao kwa ukamilifu. Hivyo, waombaji waliokamilisha taratibu za maombi ni **13,073**. Waombaji waliokidhi vigezo kwa mujibu wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya kada husika pamoja na maelekezo ya tangazo la ajira walikuwa **8,257**.

Sambamba na sifa za kimuundo, vigezo vifuatavyo vilizingatiwa wakati wa uchambuzi:-

- i. Waombaji wenye ulemavu kwa mujibu wa **Sheria ya Watu wenye Ulemavu Namba 9 ya Mwaka 2010** inayotaka **asilimia 3** ya waajiriwa wote kuwa watu wenye ulemavu,
- ii. Waombaji waliokaa muda mrefu bila ajira,
- iii. Waombaji wenye umri mkubwa,
- iv. Waombaji wa ajira wenye kada adimu.

Wizara inapenda kutoa ufafanuzi kwa hoja zilizojitokeza kama ifuatavyo:-

1. **Kuhusu waombaji waliohitimu Mwaka 2022 na kupangiwa kazi;** Hawa ni wataalam wa kada adimu kwenye soko la ajira mfano: Madaktari Bingwa, Madaktari wa Meno, Wahandisi Vifaa Tiba pamoja na Wataalam wa Radiolojia. Wataalam wa kada hizi wengi wao wamehitimu miaka ya hivi karibuni na ni wachache. Hivyo, wote waliokidhi sifa na vigezo walichaguliwa.

Aidha, Wizara imezingatia utekelezaji wa **Sheria ya Watu wenye Ulemavu Namba 9 ya Mwaka 2010** inayotaka asilimia 3 ya waajiriwa wote kuwa watu wenye ulemavu ambapo, Wizara imeajiri kundi hili kwa kuzingatia Sheria iliyotajwa hapo juu pasi na mwaka wa kuhitimu.

2. **Kuhusu kujitokeza zaidi ya mara moja kwa jina la Mwombaji;** Wizara inakiri kujirudia kwa jina la mwombaji (Agnes James Magazi, Mteknolojia Maabara) ambapo jina lilitokea mara mbili kimakosa kwenye zoezi la uchambuzi. Mhusika ametokea mara mbili kwa kupangiwa kituo cha **Hospitali ya Mkoa wa Katavi** na wakati huo huo kupangiwa kituo **Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)**. Mwombaji huyo amepangiwa **Wizara ya Ulinzi Jeshi la Kujenga Taifa** na sio maeneo mawili kama ilivyotokea kwenye tangazo. Nafasi hii itajazwa na waombaji waliopo kweye kanzidata waliokidhi sifa na vigezo kama vilivyoainishwa.

Pamoja na ufafanuzi huu wa baadhi ya hoja, Wizara inashukuru kwa hoja zilizotolewa na inaendelea kupokea maoni, ushauri na hoja mbalimbali kuhusu zoezi la ajira ili kuweza kuzifanyia kazi kwa haraka.

Wizara ya Afya inauhakikishia Umma wa Watanzania kuwa zoezi la uchambuzi wa ajira hizi lilifanyika kwa kuzingatia Sheria, Taratibu, Kanuni pamoja na miongozo iliyopo katika Utumishi wa Umma. Waombaji ambao hawakupata nafasi wasisite kuomba tena wakati nafasi nyingine zitakapotangazwa. Waombaji wanashauriwa kuwa makini wanapowasilisha maombi yao kwa kuhakikisha wanazingatia maelekezo yanayotolewa kwenye tangazo la ajira.

Imetolewa na


Englibert Kayombo

KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI